



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI  
(Barua Zote Ziandikwe Kwa Mkurugenzi Mtendaji)



**MKOZA WA KILIMANJARO**

Simu: 2755172/2751865

Fax Na. 2754305

Barua Pepe: [Ded@Moshidc.Go.Tz](mailto:Ded@Moshidc.Go.Tz)

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb. Na.MDC M.10/74

S.L.P 3003,  
MOSHI.

Tarehe: 08/01/2025.

**TANGAZO LA NAFASI YA WAJUMBE WA KAMATI YA  
HOSPITALI YA HALMASHAURI YA WILAYA MOSHI.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI  
ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUNA NAFASI YA  
WAJUMBE WA KAMATI YA HOSPITALI YA WILAYA MOSHI**

**Wajumbe wanaohitajika ni:**

- Wawakilishi wa Watumiaji wa huduma za Hospitali Watatu (3) (angalau mmoja awe wakike)
- Wajumbe kutoka Kamati za Vituo vya Afya na Zahanati za Serikali karibu na Hospitali Wawili (2)
- Mjumbe kutoka Huduma za Afya Binafsi Mmoja (1)
- Mjumbe kutoka Huduma za Afya za Taasisi za kijamii (FBOs/NGOs) Mmoja (1)

**SIFA YA MWOMBADI:**

1. **UMRI:** Kwa kuzingatia majukumu ya mjumbe wa kamati umri unaopendekezwa ni katika miaka 21 na kuendelea.
2. **URAIA:** Mjumbe wa Kamati atalazimika kuwa raia wa Tanzania. Sharti hili si la lazima kwa wajumbe kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali.
3. **ELIMU:** Waombaji wanatakiwa wawe wamehitimu elimu ya Sekondari na kuendelea.
4. Awe mwanachama Hai wa bima ya Afya (**iCHF au NHIF**)
5. Mjumbe wa kuchaguliwa ni lazima awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.
6. Mwombaji ambaye ameshatumikia kamati ya Afya kwa vipindi 3 hataruhusiwa kuomba nafasi ya ujumbe na mjumbe asiwe mwanafunzi.

## KUMBUKA:

Wajumbe wote wa kuchaguliwa hawatakiwi kuwa na nyadhifa zozote za Kisiasa kwenye Chama chochote cha Siasa wala wasiwe waajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

- Kwa maelezo zaidi wasiliana na Afisa Mtendaji kijiji, Kata au Mganga Kiongozi wa kituo cha serikali aliye karibu nawe.
- Barua zote ziandikwe kupitia Afisa Mtendaji Kijiji/Kata husika.
- Barua zote ziwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Moshi

### **Mkurugenzi Mtendaji (W)**

**S.L.P. 3003,**

**MOSHI.**

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30.01.2025.**

  
Shadrack M. Mhagama.  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MOSHI**

  
Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
Moshi

Nakala:

Mkuu Wa Wilaya,  
S.L.P 3043  
**MOSHI.**

- *Kwa Taarifa*

Mamlaka ya Mji Mdogo,  
S.L.P 3003,  
**MOSHI.**

- *Kwa Taarifa*

Watendaji Wa Kata Zote,  
S.L.P 3003,  
**MOSHI.**